



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD**

Tuesday, 24th February, 2026

Third Assembly – Fifth Session
FOURTH SITTING

*[The County Assembly met at 2:33p.m at the County Assembly Buildings]
[The Speaker (Hon. Aharub Ebrahim Khatri) in the Chair]*

PRAYERS

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Members, you may be seated. Clerk, please confirm if we have the quorum.

[Lack of quorum]

Honourable Members, according to Standing Order 31(2):

If there is no quorum present when the Chair is taken, if there is no quorum present when the Chair is taken at the time appointed for a meeting of the County Assembly, immediately after the saying of the prayers the Speaker shall order the bell to be rung for 10 minutes and if no quorum is present at the expiration of the ten minutes the Speaker may direct that the bell be rung for a further five minutes and if there is still no quorum present the Speaker shall adjourn the County Assembly forthwith to the next sitting.

Serjeant-At-Arms, please ring the bell for ten minutes.

[Serjeant-At-Arms rung the quorum bell for ten minutes]

[A few Honourable Members walked in]

Yes, Clerk please confirm if we have the quorum?

[Client confirmed quorum]

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Clerk next order please.

PAPERS

REPORTS OF THE AUDITOR GENERAL ON COAST GENERAL TEACHING AND REFERRAL HOSPITAL FOR THE YEARS ENDED 30TH JUNE, 2022, 2023, 2024, FOR THE COUNTY GOVERNMENT OF MOMBASA

Yes, Leader of the Majority Party please lay down the Paper.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you, Mr. Speaker Sir. Mr. Speaker Sir, I wish to lay Paper reports of the Auditor General on Coast General Teaching and Referral Hospital for the years ended 30th June, 2022, 2023, 2024, for the County government of Mombasa.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Leader of the Majority Party, for laying down the Paper. Honourable Members, the report of the Auditor General on Coast General Teaching and Referral Hospital for the years ended 30th of June, 2022, 2023, and 2024 for the County government of Mombasa stands committed to the County Public Accounts and Investments Committee for consideration. Yes, Clerk next order please?

REPORT OF THE AUDITOR GENERAL ON MOMBASA COUNTY ALCOHOLIC DRINK CONTROL FUND FOR THE YEARS ENDED 30TH JUNE, 2025

Yes, Leader of the Majority Party please lay down the Paper.

The Leader of Majority (Hon. Khatri): Thank you, Mr. Speaker Sir. Mr. Speaker Sir, I wish to lay Paper report of the Auditor General on Mombasa County Alcoholic Drink Control Fund for the years ended 30th June, 2025.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, thank you very much Honourable Majority Leader for laying the Paper. Honourable Members, the report of the Auditor General on Mombasa County Alcoholic Drink Control Fund for the years ended 30th June, 2025 stands committed to the County Public Accounts and Investments Committee for consideration. Yes, Clerk, next order please.

REPORT OF THE AUDITOR GENERAL ON COUNTY GOVERNMENT OF MOMBASA FOR THE YEAR'S ENDED 30TH JUNE, 2025

Yes, Leader of the Majority Party please lay down the Paper.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, I wish to lay Paper report of the Auditor General on County government of Mombasa for the years ended 30th June, 2025.

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Members, the report of the Auditor General on County Government of Mombasa for the years ended 30th June, 2025, stands committed to the County Public Accounts and Investments Committee for consideration. Yes, Clerk next order please.

REPORT OF THE AUDITOR GENERAL ON MOMBASA INVESTMENT CORPORATION FOR THE
YEAR ENDED 30TH JUNE, 2025

Yes, Leader of the Majority Party please lay down the Paper.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, I wish to lay Paper; Report of the Auditor General on Mombasa Investments Corporation for the years ended 30th June, 2025.

[Paper laid]

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Members, the Report of the Auditor General on Mombasa Investment Corporation for the years ended 30th June, 2025 stands committed to the County Public Accounts and Investment Committee for consideration. Yes, Clerk next order please?

MOMBASA COUNTY PUBLIC SERVICE BOARD ANNUAL REPORT FOR THE YEAR, 2024/2025

Yes, Leader of the Majority Party please lay down the Paper.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, I wish to lay Paper Mombasa County Public Service Board Annual Report for the year 2024/2025.

[Paper laid]

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Members, the Mombasa County Public Service Board Annual Report 2024 - 2025 stands committed to the Committee on Labour and Public Service Administration for consideration. Yes, Clerk next order please.

THE 2024/2025 EVALUATION REPORT ON THE EXTENT TO WHICH THE COUNTY PUBLIC SERVICE HAS
COMPLIED WITH VALUES AND PRINCIPLES IN ARTICLE 10 AND 232 OF THE CONSTITUTION-LEADER
OF MAJORITY

Yes, again, Leader of the Majority Party.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, I wish to lay Paper, the 2024 - 2025 Evaluation Report on the extent to which the County Public Service has complied with values and principles in Article 10 and 232 of the Constitution of Kenya.

[Paper Laid]

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Members, the report the evaluation of the extent to which the County Public Service has complied with values and principles in Article 10 and 232 of the Constitution stands committed to the Committee on Labour and Public Service Administration for consideration. Yes, Clerk next order please.

NOTICE OF MOTION**ADOPTION OF REPORT ON THE PUBLIC SERVICE ADMINISTRATION ON THE MOMBASA COUNTY
REVOLVING FUND BILL, 2025**

Yes, Honourable Jactone Madialo please give the Notice of Motion. Yes, Honourable Bernard Ogutu?

Hon. Ogutu: Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker, I'm standing in for the Chair. Mr. Speaker Sir, I beg to give a notice of the following Motion...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Are you a Member of that Committee?

Hon. Ogutu: Yes.

The Speaker (Hon. Khatri): Okay.

Hon. Ogutu: Thank you. Mr. Speaker Sir, I beg to give a notice of the following Motion.

THAT this House adopt the Report by the Committee on Labour and Public Service Administration on the Public Participation for Mombasa County Revolving Fund Bill, 2025 laid on the Table on Tuesday, 24th February, 2026 during the third sitting.

Thank you.

MOTIONS**INVESTIGATION INTO THE MANAGEMENT AND OPERATIONS OF COAST GENERAL TEACHING
AND REFERRAL HOSPITAL**

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Katana please give the notice of Motion.

Hon. Katana: Thank you, Mr. Speaker Sir. I stand to give the following notice of Motion; Investigation into the management and operations of Coast General Teaching and Referral Hospital. Mr. Speaker Sir,

AWARE THAT Article 43(1) (a) of the Constitution of Kenya guarantees every person the right to the highest attainable standard of health, including the right to health care services.

FURTHER AWARE that Coast General Teaching and Referral Hospital is the principal public referral health facility serving residents of Mombasa County and the coastal region at large.

COGNIZANT THAT, recent reports in the public domain indicate that the Chief Executive Officer of the hospital, Dr. Iqbal Khandwalla, has been suspended amidst allegation of malpractice, administrative irregularities and mismanagement within the facility.

Mr. Speaker,

DEEPLY CONCERNED THAT there have been complaints from members of the public alleging negligence in service delivery, which has allegedly resulted into loss of life and declined standard of care at the hospital.

ALSO CONCERNED THAT the circumstances surrounding the suspension of the Chief Executive Officer has raised questions regarding due process, governance, accountability and the overall management structure of the hospital.

Mr. Speaker, I therefore ask this Honourable House to resolve that;

The County Assembly Committee on Health undertake a comprehensive enquiry into the management, administration and operations of the Coast General Technical Teaching and Referral Hospital.

Number two, Mr. Speaker, the Committee investigate the allegation of negligence, malpractice and loss of life attributed to operational failure at the hospital.

Number three, the Committee examine the circumstances leading to the suspension of Dr. Iqbal Khandwalla and determines whether due process was followed and whether the suspension was lawful, justified and the best interest of the public service.

Mr. Speaker, number four, the Committee engages relevant stakeholders, including the County Executive Committee, Members for health, the hospital board, staff representatives and Members of the public and receive written and oral submission.

Lastly, Mr. Speaker, the Committee tables before this Assembly, within a period of seven days, a comprehensive report containing its findings, recommendations and proposed remedial measures to restore public confidence and improve service delivery at this hospital.

Thank you, Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much, Honourable Allen Katana from Shanzu Ward. Yes, Clerk, next order please that was a notice of Motion. That was a notice...

[Loud consultations]

So now we go to Motion. So that was a Notice of Motion. Next order, Clerk?

INVESTIGATION INTO THE MANAGEMENT AND OPERATIONS OF COAST GENERAL TEACHING
AND REFERRAL HOSPITAL

Yes, again Honourable Allen Katana, MCA Shanzu Ward. You can now move the Motion?

Hon. Katana: Thank you, Mr. Speaker for giving me this time so that I can now read it as a Motion because it first came as a Notice. Mr. Speaker, the Motion is; *investigation into the management of the operations of Coast General Teaching and Referral Hospital*. Mr. Speaker Sir, I beg to move the following Motion;

AWARE THAT Article 43(1)a) of the Constitution of Kenya guarantees every person the right to the highest attainable standard of health, including the right to health care services.

FURTHER AWARE THAT Coast General Teaching and Referral Hospital is the principal public referral health facility serving residents of Mombasa County and the coastal region at large.

COGNIZANT THAT recent reports in the public domain indicate that the Chief Executive Officer of the hospital, Dr. Iqbal Khandwalla, has been suspended amidst allegations of malpractice, administrative irregularities and mismanagement within the facility.

Mr. Speaker, DEEPLY CONCERNED THAT there have been complaints from members of the public alleging negligence in service delivery, which has allegedly resulted into loss of life and declined standard of care at the hospital.

ALSO CONCERNED THAT the circumstances surrounding the suspension of the Chief Executive Officer has raised questions regarding due process, governance, accountability and the overall management structure of the hospital.

Mr. Speaker, I therefore ask this Honourable House to resolve that;

The County Assembly Committee on Health undertake a comprehensive enquiry into the management, administration and operations of the Coast General Technical Teaching and Referral Hospital.

Number two, Mr. Speaker, the Committee investigate the allegation of negligence, malpractice and loss of life attributed to operational failure at the hospital.

Number three, the Committee examine the circumstances leading to the suspension of Dr. Iqbal Khandwalla and determines whether due process was followed and whether the suspension was lawful, justified and the best interest of the public service.

Mr. Speaker, number four, the Committee engages relevant stakeholders, including the County Executive Committee Member for Health, the hospital board, staff representatives and members of the public and receive written and oral submission.

Lastly, Mr. Speaker, the Committee tables before this Assembly, within a period of seven days, a comprehensive report containing its findings, recommendations and proposed remedial measures to restore public confidence and improve service delivery at this hospital.

Honourable Mr. Speaker, for those so many remarks. Mr. Speaker, I will therefore, honourable ask Honourable Abdirahman to second this very important Motion. Thank you, Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Katana *IGB*.

Hon. Abdirahman Abdikadir: Mr. Speaker, with your permission allow me to second this Motion.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you, Honourable Abdirahman Hussein. Honourable Members, I now propose the question that the Motion by Honourable Allan Katana be considered by this Honourable House in the same terms as moved?

[Question proposed and agreed to]

And yes, Honourable Allen Katana, please make your contribution to this Motion?

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika kwanza nilishukuru Bunge hili na pili nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kutupa ruhusa ili tuweze kujadili swala hili. Nimekuwa katika vyombo vingi vya habari nikitetea maswala na utenda kazi wa hospitali yetu ya Makadara na Mheshimiwa Spika hapo nyuma kwa muda mrefu nilipokuwa nikipiga kelele kuhusu utenda kazi na huduma zinazotolewa pale Makadara watu wengi waliniita mimi kama mwenda wazimu. Wengine Mheshimiwa Spika wakaleta kwamba ni maswala ya kisiasa lakini pale ndani imejitokeza vizuri ya kwamba wananchi wetu wana matatizo. Mheshimiwa Spika imekuwa juzi tu maana nakumbuka Mheshimiwa Spika tukiwa na wewe Likoni nilitoa na ahadi kwamba tutakapo rudi baada ya mapumziko ni lazima ajenda inayohusu maswala ya Makadara yaweze kuingia Bunge na nataka kutoa shukrani ya kwamba Mwenyezi Mungu amenisaidia ajenda ile ile hivi sasa pamoja na Waheshimiwa wenza tutajadili hapa Bunge.

Mheshimiwa Spika swala la leo ni kwamba daktari mkuu anayesimamia hospitali ya Makadara ametolewa katika wadhifa ule kisa na maana ripoti tunazopata ni kwamba kumekuwa na utepetevu katika kutoa huduma, tena ripoti zinasema imemhusu moja kwa moja Daktari Khandwalla ndiposa nimeleta maombi haya ndani ya Jumba hili ya kwamba kupitia Kamati yetu inayoongozwa na Mheshimiwa shemeji yangu Ogutu wakaweze kufanya utafiti; je malalamiko haya yaliyoletwa kwa Daktari mkubwa moja kwa moja ni ya kweli ama ni ya uongo na mimi nimeshtushwa sana Mheshimiwa Spika na hili utaniruhusu kwa heshima ya Jumba hili nilitaje. Mimi kama Katana pamoja na waheshimiwa wengine kwenye Jumba hili tumekuwa tukilalamikia kuhusu utenda kazi wa hospitali ya Makadara Mheshimiwa Spika lakini Mstahiki Gavana hakuna hatua yoyote aliyofanaya ilikuwa anangoja Gavana mpaka mtu aliyekaribu naye atendeke na kitu fulani ndio achukue hatua ya kuwasimamisha watu kazi Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, jambo hilo mimi ndilo nililotuma mpaka leo hii nilete hoja hii tukaweze kuijadili hapa, kumekuwa na vilio vingi ni watu wangapi walikuwa wasubiriwe wafe ndio *wing* ile ya *executive* itoe njia muafaka ya kuweza kuwasaidia watu Mheshimiwa Spika lakini kwa kuwa kila kilicho na mwanzo kina mwisho na hoja hii imeingia ndani ya nyumba hii Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika nisiwe mwingi wa maneno maana nitakuwa mwisho wa kusherehesha niwaache Waheshimiwa wenza ili nao wakaweza kutoa hoja zao kulingana na wanavyo liona swala hili. Lakini ukweli ni kwamba Mheshimiwa Spika watu wetu wanateseka pale Makadara, watu wetu hawapati huduma zinazostahili, watu wetu pale Makadara wamepewa hata ahadi na kwa kuwa kwa mujibu wa *Kanuni zetu za kudumu* 87 imesema Mheshimiwa

asisimame hapa atoe hoja ambayo si ya kweli. Mheshimiwa Spika, mimi nataka kutoa hoja ya ukweli hata serikali yetu ya Kaunti ambayo inaongozwa na Mstahiki Gavana Abdulswammad aliwahi kuleta *policy* ya kusema anayekuwa na mgojwa wake kuanzia miaka sufuri mpaka mitano atakuwa anapata huduma bure. Lakini leo hii Mheshimiwa Spika wewe ni shahidi maana una shida pale hospitali ukisaidia wakaazi wa Mombasa huduma hii imekuwa inapatikana ki nadra. Mheshimiwa Spika kunayo Hoja ya *waiver* hatujui ni *criteria* gani inatumika kupeana hiyo *waiver*, pale kuna wagonjwa wengine hawawezi hata kujikuna lakini wanaambiwa wabaki peke yao kwa Wadi. Mheshimiwa Spika, nikiongea nitachukua muda hata wa wenzangu maana yako mengi yanayo huzunisha mimi ningeomba nikurudishie ili wenzangu nao wakaweze kuchangia katika mjadala huu ili mwisho wa kwisha watu wetu wa Mombasa wakaweze kupata natija. Shukran Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Ahsante sana Mheshimiwa Katana *IGB*. Naam, Mheshimiwa Ibrahim Omondi kutoka Airport Wadi tafadhali to mchango wako?

Hon. Omondi: Thank you Mr. Speaker for catching up with my eye. It is true Mr. Speaker, that this Motion is a very great concern not only to the Mombasa County residents but it goes further because you know that even other Counties benefit from the same facility therefore if Coast General goes down then it will mean it will go down with very many lives that is why I want to support a hundred support the Motion that is in the floor...

[Applause]

But what has happened we want to urge the Committee to take it very seriously because it is not a joke Mr. Speaker; a human life you can joke with any other thing but not something that concerns human life, health care, health care Mr. Speaker is not a profit-making scheme. It is not; we should understand that Mr. Speaker for some shadow interest it is a constitutional facility and it is a constitutional obligation that each and every person should receive health care. Number two; Mr. Speaker, the referral facility which is Coast General Hospital remains a very critical pillar, of the health care serving not only the Mombasa but also other Counties as I have explained and therefore the government of the day that is the County government of Mombasa should ensure and should strengthen system Mr. Speaker that will enhance patient safety and also sustaining public confidence. Mr. Speaker, is contrary to what has happened because when I look at the social media, when I look at the magazines and I look at the TVs that is the matter which is being discussed currently and therefore this House Mr. Speaker has an authority that has been given by the Constitution to ensure that the right thing is done.

Mr. Speaker, I remember three years ago there was a problem at the Coast General Hospital and I remember when I was somewhere enjoying my drink from a famous hotel around, I received your call and you told me Mr. Ibrahim Omondi there is a problem at the Coast General I think that at that particular time the power in that particular facility had been switched off. I rushed there and I found the Committee was already in and other Members, concerned Members in that particular facility. Mr. Speaker, it was suicidal; the whole facility, the power had gone down and that one had even affected some of the patients which were told even it led to the loss of some of the patient; these are the issues that we are talking about, this negligence that should not repeat and should not be coming. Mr. Speaker, some patients have been complaining some families have been complaining that when they go to the facility they are told to go and buy or purchase medicine from the external pharmacies while we all know that the facility should be able to provide the medicine in the facility.

Mr. Speaker, we want to know and this is now where I want to end, if we did the suspension of the CEO the one Mr. Khandwalla is really, had really followed the law and this should not be a divert or should not divert the attention from the deeper network of influence, we actually Mr. Speaker what you are trying to say that the public will not accept the scapegoat while the real beneficiary of alleged irregularities remain untouched. Mr. Speaker, let the Committee become very serious about this investigation and let us know if there is something which is deeper than what we have seen today, if there are some politicians I want to mention that who are beneficiary and who are interfering with the working of that particular facility. Mr. Speaker, thank you. As I await the report from the Committee...

[Applause]

I just want to promise the Chair of the Committee that if we are not going to get good results from this House we are going to go down with you Chair! Thank you very much.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Ibrahim Omondi from Airport Ward. Yes, Honourable Abdirahman Hussein from Mji wa Kale Ward. Please make your contributions to the Motion.

Hon. Abdirahman Abdikadir: Thank you Mr. Speaker Sir. On a lighter note, Mr. Speaker, I want to quote one of the many phrases attributed to PLO Lumumba. Professor PLO Lumumba once said that;

'If you take away the phrase, the filler word Mr. Speaker Sir, from the context from the speeches of Honourable Members the speeches will leave little to be desired'.

Mr. Speaker, I do not wish to divulge much on that but rather let me get into the Motion of the day, the Motion is not timely but I can say better late than never. This is an issue or rather an incident that has happened four days ago much in the public domain a lot has been said Mr. Speaker but our legislative voice was missing from the conversation and I would like to applaud my colleague Honourable Katana for finding it fit to come up with a substantive Motion to discuss what transpired and in to get deeply into the efficiency or lack of efficiency of services at the Coast General Hospital. Mr. Speaker, a life lost is one too many and it saddens me as it saddens the rest of my colleagues that indeed we have had a lot of hue and cry from the members of the public about the service and the level of service delivery at the Coast General. I am a frequent visitor of Coast General, I have seen it for myself the suffering, I have seen it for myself the cries whether it comes to services received from there or rather due to the inflated bills that we have seen and we as legislators have taken it upon ourselves to review those charges. Mr. Speaker, the Coast General does not only serve the residents of Mombasa it serves the wider Coast all the way from Tana River to Lamu, from Kilifi to Kwale every patient runs to Coast General and it's paramount and it's very imperative that we as legislators ensure that the services offered at the Coast General is of the highest standard.

Mr. Speaker, the very unfortunate incident that happened four days ago that needs our attention is one that really shocked me when I saw the Member of Parliament from Mvita as he went there and made claims that one the CEO Mr. Iqbal Khandwalla has been accused of gross incompetency and misconduct. Mr. Speaker, this is a matter that needs our attention; the attention of the House through the Committee, the Committee on Health they need to take this matter with a lot of seriousness and as such I cannot add more to the five prayers that the mover

of the Motion has suggested. Mr. Speaker, we do not need to take much of time or rather we do not need to take more than a week to conclusively deal with this matter I have read a lot on social media and I have seen it a lot but as a Legislative House we need to get to the bottom of this matter. We need to know whether the CEO is culpable of any gross misconduct, we need to know whether the board were in their right powers to dismiss him from that position and go much deeper and ensure that we have efficiency at the level of service delivery in Coast General Mr. Speaker. With those few remarks Mr. Speaker allows me to support this Motion with all the gravity that it deserves. Ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Abdirahman Hussein. Yes, Honourable Prischillah Mumba please make your contribution.

The Chief Whip (Hon. Mumba): Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia mchakato huu wote unaoendelea wa hospitali ya Coast General na nimesimama hapa kuunga mkono kikamilifu Mheshimiwa Allen Katana ambae kwa Bunge hili watu wanajua ni bwanangu lakini leo namuunga mkono kama Mheshimiwa aliyeleta Hoja ya muhimu sana, na kwa nini nasema hivyo? Jambo hili Mheshimiwa Spika si mara ya kwanza, wala ya pili wala ya tatu wala ya kumi kuja ndani ya Jumba hili. Mheshimiwa Spika, tulipokua tukileta Hoja tofauti tofauti kupitia tetesi za wananchi wanazo tuletea kwa sababu hata sisi tumechaguliwa na tunaongoza watu ambao wanahudumiwa katika ile ile hospitali na wakati tulipokua tukiletewa zile tetesi na tunajaribu kuja kutoa sauti yetu hapa kwa sababu ndio ki sheria lazima tupitie katika Bunge kutoa Hoja na kusema tetesi zetu ndipo sasa ziweze kunukuliwa ziweze kupelekwa kunako stahili ili marekebisho yaweze kufanyika. Lakini kwa masikitiko tumekua tukipitisha mambo haya mengi yanayofanyika katika hospitali ya Coast General lakini tulikuweko hatuoni mabadiliko yeyote. Mimi langu ninalo tamaushwa nalo ni moja tu, ilikua inastahili itoke sauti ya kiongozi ambaye ni wa kutoka Bunge Kuu ndio sasa mchakato uwe kuchakatwa jinsi ulivyo?

[Applause]

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge pia nimechaguliwa katika nyanja ya chini lakini ninapotoa sauti katika Bunge la Kaunti ama katika Kaunti hii hawa Waheshimiwa unao waona wamekaa hapa hata tukatoa sauti gani ilikua sauti zetu hasikizwi. Lakini leo kumetokea sauti ambayo imesikizwa na namshukuru Mungu maana siku zote ngoma ikipigwa sana hupasuka na ngoma ishapasuka kwa sababu yanayoendelea hospitali ya Coast General si urongo ni ukweli mtupu. Mimi haswa kama kiongozi nimekutana na matatizo tofauti ambayo nimepeleka watu wangu wakinililia kuweza kuwasaidia na yakatushinda kwa sababu njia tunazo zipitia hata utakapokwenda utakapo sikizwa kama kiongozi pia unapuuzwa pale mgonjwa atakwenda ataambiwa ainuke mwenyewe kitandani aende akaangalie SHA kama yake imekua *activated*. Mgonjwa ametoka chumba cha upasuaji atajua vipi ni mpaka ateremke kule chini aende akasema kwa SHA kuwa nimetoka kwenye chumba cha upasuaji ndipo sasa aweze kulipiwa ati ile SHA. Vile vile mgonjwa huyu anaweza kua pengine hajiwezi wana hana ufahamu wa kutakikana kufanyike nini na nini katika sheria za hospitali; leo haelezwi Mheshimiwa Spika anawachwa anaingia, anahudumiwa, anakaa baada ya siku mbili siku tatu anaambiwa wewe hukuenda kuripoti kwa SHA. Kwa hivyo SHA haiwezi kukulipia; huyu mgonjwa alikuja yuko hali mahututi Mheshimiwa Spika, alikua hana ufahamu wa kujua kuna SHA wala hakuna SHA, yeye alikua ameletwa pale kuokoa maisha yake alikua na ufahamu gani kua mpaka aende akajiandikishe kwa SHA yeye aliletwa na machera akiwa hana fahamu? Wajibu wa kua wale

walio mpokea ndio waende pale kwa SHA wakaseme hilo halikufanyika lakini wakati mgonjwa sasa anataka kutoka katika bili ndio anaambiwa wewe huwezi kupiliwa na SHA kwa sababu hukuripoti ile siku uliyoingia na alipoingia alikua ni mtu hana fahamu, alikua aripoti vipi?

Hayo ni matatizo yanatokea hospitali ya Coast General. Coast General hii umetibu mtu, amekuja amekwambia mimi kiwango nilicho nacho bili yangu ni Kshs.50,000.00 mimi kiwango nilicho nacho ni Kshs. 30,000.00 ama Kshs.20,000.00. Wajibu wa kua huwezi kumtoa yule mgonjwa ni mpaka alipe lile deni waendelea kumuweka pale bila kumuambia pia nenda ukasimamishe ile bili yako maana yake hana ufahamu yeye kujua mpaka hapo alipotolewa. Sasa nenda kwa pahali husika usimamishe ile bili pia haambiwi anaachwa tu amekaa kwenye Wadi amepewa ruhusa ya kutoka na kwa sababu hana pesa inakua ile bili yake inaendelea kupanda wakati atakapokua anakuja anasema mimi nadaiwa Kshs.50,000.00 Mheshimiwa Spika anakuta bili yake ishafika laki moja yeye anarudi anashindwa mimi nilipewa ruhusa ya kutoka na elfu hamsini, laki moja imetokea wapi? Anaambiwa hukuenda kusimamisha bili yako. Huyu mgonjwa alikuwa na fahamu gani ya kujua aende asimamishe ile bili yake? Na wewe unajua shida ni kulipa pesa.

Saa hizi hivi ninavyokuambia Mheshimiwa Spika mimi juzi nakushukuru umenitolea maiti yangu ambayo ilikua imekaa mwezi mmoja na wiki mbili ambapo ikuwako ni bili ya *mortuary* na mtu ameshindwa kulipa. Saa hii ninavyokuambia kuna bili nyengine ya mtu amekaa hapo miezi miwili na mwenye kufiwa ni askari gongo anayefanya kazi ambaye mshahara wake analipwa shilingi elfu tano ana bili ya elfu arobaini na tano na mwili umekaa hapo miezi miwili na hata ukitaka nitakutolea ushahidi niko nao. Niambie askari huyu ambaye nimeenda nikajua mshahara wake ni elfu tano ana bili ya mke wake elfu arobaini na tano ana miezi sasa miezi mwili umekaa *mortuary* ambapo ameshindwa kutoa mwili na mtu huyu ni mwanadamu Mheshimiwa Spika anaishi, anakula, analala nyumbani, anatoka asubuhi anaenda kufanya kazi yake ya uaskari akijua bibi yake yuko *mortuary* na ameshindwa kumtoa. Hebu niambie hayo mateso ya huyo mwanadamu anayopitia na hana kiongozi yeyote ambaye anayeweza kumtolea sauti kama hivi leo hapa mimi nimesimama hapa ndani ya Bunge naeleza jambo hili.

Mheshimiwa Spika kuna mambo ya kusikitisha katika hospitali ya Coast General na si mambo ambao sisi viongozi tunashindwa kuhudumia ikiwa kiongozi amekuja pale na anasema mimi naomba huyu mtu wangu atolewe, mimi nitakua nikitoa hata kama ni Kshs.5,000.00 kila mwezi chukua stakabadhi zangu. Mheshimiwa Spika, hakuna mtu anayesikiza na halafu tunashangaa kusikia ati muungano wa madakitari unaungana kusema tunapinga kutolewa kwa dakitari huyu, tunapinga Waheshimiwa kuingilia maswala ya hospitali ya Coast General. Mheshimiwa Spika mimi nimechaguliwa na mwananchi na wakati huyu mgonjwa anaepolekwa pale ni mtu ametoka katika Wadi yangu, hakuna haki mimi kama kiongozi kumsema? Ama kumsaidia? Leo wao wanasema hivyo na kuna baadhi ambao wako katika hio hio hospitali ya Coast General tuliwapitisha sisi katika hii Nyumba, wakati walipokuwako tukiwapitisha hawakujua sisi ni wanasiasa?

Leo hii kwa vile sasa imetokea kuna matatizo na tunataka kuadhibu watu ambao tunaona wamezembea na kazi yao sasa imekua waheshimiwa waliochaguliwa kisiasa hawatakiwi kuingilia kazi zetu. Kazi yao ni nini ikiwa tunaona mambo ya aibu yanatokea kama haya? Kazi yao ni nini katika County Government maana kuna mambo mpaka ya ndani yamenukuliwa kua Waziri pia anasema Dakitari Iqbal Khandwalla ametushinda, Chief Officer nae yuwasema Dakitari Iqbal Khandwalla ametushinda. Sasa mtu mmoja huyu ni zaidi ya Raisi? Hata huyu Raisi, Mheshimiwa Ruto *is not above the law*; ikiwa kuna sheria ya kua inaruhusu kua aulizwe kwa nini haya yaliyotokea yametokea sioni kua kuna makosa, lakini Mheshimiwa Spika jana na juzi hatukua katika maandamano. Lakini hapa natoa tahadhari kabisa maandamano ya kuanzia kesho mimi niko hapo kwa sababu wasitutishie viongozi ati hatufai kwenda kwenye

maandamano kwa vile wananchi wanapiga makelele tuogope madakitari hao, madakitari wote katika hospitali ya Coast General hatuwataki na waende wacha watu wetu wafe mpaka tutakapopata madakitari wengine waingie waweze kuweza kuwajibika wametuharibia sura ya Mombasa, wametuharibia viongozi, wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika tumekua na wewe pale hospitali ya Coast General ukipigana vita ukitoa miili ambayo imekaa zaidi ya mwezi mzima Mheshimiwa Spika nilikushuhudia mwenyewe na macho yangu ukiandika bili *cheque* na kutoa watu kama ambae ni kazi yako na si kazi yako, kwa sababu miili imejaa *mortuary* imejaa mpaka inafurika nje miili haijui iwekwe wapi kisa na maana Kaunti inatafuta pesa. Mwatafuta pesa kwa wafu hata yule masikini ambae hana pesa tutafanya nini Mheshimiwa Spika na mambo makubwa tunasingiziwa ati sisi Mheshimiwa Spika tulipitisha katika Jumba hili bei za juu hospitali ya Coast General.

Mheshimiwa Spika sasa sisi hapa tulipopitisha tulikua wazuri lakini wakati sasa twawabwaga tutakua wabaya basi tushakubali kuwa wabaya maana safari hii iwe ni jambo gani lolote litakalo kuja ndani ya Jumba hili kama haitapita kwa sufuri basi itapita kwa moja maana tumechoka kuona unyanyasaji wa watu wa Mombasa. Sisi kama viongozi tunyamaze ama sisi kama viongozi tukisema tunakuja tena tunatukanwa tena kwa ajili ya kuzungumza. Tulipozungumza tuliambiwa mbona mukifanyiwa mengine hamusemi. Ni yapi hayo tunayofanyiwa ambayo ndio leo hapa tushindwe kuyasema? Leo ikiwa watu wetu wafa tunyamaze? Ama watu wafa tusizungumze? Haya basi katika hesabu ya Mbunge wangu ikiwa Mbunge wangu alizungumza akanukuliwa ni mbaya na mimi pia niko kwenye hio hesabu ninukuliwe leo mimi ni mmbaya na nashukuru Mheshimiwa Spika umetuwekea hivi vifaa viko hapa vina nukuu tunaonekana live tunavyoponda na kuzungumza na nitaendelea kuponda mpaka dakika ya mwisho.

Mimi siuungi mkono, siuungi mkono hata huyo dakitari ambaye anayesema anataka maandamano kesho atanikuta mimi hapo nikiamua *he must go* na hatarudi katika Kaunti ya Mombasa asitutishie kwa sababu yeye ndie amefanya madhara haya yote yakatokea. Kiongozi hawezi kusimama akawa ni mwendawazimu akizungumza asieleweke; amezungumza maneno ya kueleweka Dakitari Iqbal Khandwalla huna kazi unayofanya katika hospitali ya Coast General na huo ndio ukweli wa mambo huwezi kutuulia watu wetu katika Mombasa halafu tunyamaze. Wewe utakwenda na kama hukwenda waheshimiwa wenzangu kuanzia kesho hakuna kuingia hili Bunge ni maandamano tukeshe pale hospitali ya Coast General mpaka tuhakikishe fagilio zote zimeenda. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Kibwana Swaleh?

Hon. Kibwana Swaleh: Mheshimiwa Spika nimeona mwenzangu anaongea na jazba na ningeomba Mswada huu tukiongea na jazba hatutapata suluhisho na mimi ilikua nataka kusema haya maoni ambayo yamewekwa hapa na ndugu yetu Mheshimiwa Allen Katana ambaye in *IGB* ni mambo ambayo tungengoja ile ripoti kamili ikija ndio tuweze kutathmini zaidi na Mheshimiwa Spika huyu CEO hatuwezi kumshutumu kama tunavyofanya kwa sababu ni lazima tumpe nafasi pia ya kujielezea, lakini tukiendelea hivi na mjadala tutakua tushamhukumu na yale mambo ninayo yasikia kwenye mitandao ni tahadhari. Mheshimiwa Spika huyu ni binadamu na licha ya mapungufu amefanya kazi kubwa pale hospitali ya Coast General; ile hospitali ya Coast General iliyokua tunaijua kule nyuma si vile iko. Kwa hivyo hiki kitendo na si hiki pekee kuna watu washakufa lakini hakujakua na kelele kama hizi. Haiwezi kuwa ni Mbunge ndio amesema sasa kila mtu yuwamlaani, wangapi wamekufa na hatukusikia watu wakilalamika. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika maombi yangu ndani ya Nyumba hii, ni Nyumba ya kisheria, ni Nyumba wenye nidhamu tumpe *a second chance* tuipe Kamati ambayo itazama chini ki utaalumu na

kiufundi kutupatia ripoti ambayo tutaweza kuijadili kwa hivyo ningesema tu nataka ninukuliwe kwamba tumpe *fair hearing the CEO* ili nae pia tumsikize. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Kibwana Swaleh. Honourable Kibwana Swaleh that was your contribution to the Motion?

Hon. Kibwana Swaleh: Yes.

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Frankline Makanga from Chaani Ward?

Hon. Makanga: Thank you Mr. Speaker, and with your permission I make my contribution in Kiswahili. *Mheshimiwa Spika, kwanza natamaushwa na vile Waheshimiwa wenza wanataka kulichukulia swala hili; hili si jambo la kuweka mihemko ya kihisia na hili pia si jambo la kuweka ili tujione kwa mitandao kwamba tumesema katika Bunge. Maswala yanayo husiana na utenda kazi wa hospitali ni maswala ambayo Bunge hili limefuatilia, tumezungumzia ikiwemo Mheshimiwa Spika taarifa ambayo ilikua inaitwa the Mombasa Health Task Force Report ambayo pesa za ummah zilitumika mwaka 2023 kuweza kutengeneza Kamati ambayo ilitayarisha ripoti ambayo ilikua ya kueleweka ambayo ilianguzia ni jinsi gani hospitali zetu ikiwemo hospitali ya Coast General itaweza kufanya kazi. Mheshimiwa Spika iingie katika kumbukumbu ya Bunge hili kwamba sisi hatuko hapa kutangaza maandamano hio sio kazi yetu na kama itafanywa nje na wanasiasa lakini hapa tukiwa watenda kazi tunawakilisha wakiwemo wale ambao wanaonekana kuwa na makosa.*

Pili, Mheshimiwa Spika katika maombi ambayo yameletwa yakielekezwa katika Kamati ya Afya ambapo mimi nina kaa ni kwamba hayo ambayo wangetaka Kamati iweze kuangazia yako katika majukumu yetu na yako kisheria na Mheshimiwa Spika kabla sisi hapa tupitishe hukumu ieleweke ya kwamba hata hio Bodi ya hospitali ya Coast General ambayo wanasema imemsimamisha kazi hawana majukumu hayo kisheria Mheshimiwa Spika. Kwa hivyo tunavyozungumza hapa kufurahia kwamba amesimamishwa kazi tujue kwamba sheria tayari ishavyunjwa na hio Bodi ambayo inasimamia usimamizi wa hospitali ya Coast General kwa hivyo Mheshimiwa Spika wasia wangu na maombi yangu ni kwamba wanasiasa wa Mombasa na uongozi ukiongozwa na Gavana wasilichukulia swala hili la kuwapa bloggers wao kutukana viongozi na kuweka misimko ya kisiasa na kihisia bila kuangazia...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Josh Ong'ao?

Hon. Ong'ao: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity. I want to inquire what does the mover of the Motion, what are the pleas of the mover of the Motion?! Is whatever Members are discussing here are among the pleas that the mover of the Motion has requested for? We are discussing, it is like we are discussing a report that we do not have. Can we stick to the Motion? Thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Joshua Onga'o. That was a point of information, right?

Hon. Onga'o: Yes.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you. Yes, Honourable Frankline Makanga you can continue.

Hon. Makanga: Mheshimiwa Spika naona swala hili limefanya hata waliokua hawazungumzi wanazungumza...

[Laughter]

Kwa hivyo tunashukuru kwa hilo. Mheshimiwa Spika naomba niendele...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Continue please.

Hon. Makanga: Kwa hio Mheshimiwa Spika mimi nilikua naomba ya kwamba swala hili...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Athman Mwamwiri?

The Leader of the Majority Party (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika katika lugha fasaha unaposema wasiozungumza unamaanisha walemavu wa sauti ambao ni mabubu, sasa pengine Mheshimiwa atuthibitishie katika Bunge hili kama angalau kwa bahari mbaya ama nzuri tunae mwakilishi ambae kimaumbile ni bubu na leo kwa miujiza ya hoja hii, Mungu kamtendea kamuonea na yeye sauti imefungika pasi na maombi, pasi na matibabu na yeye anazungumza...

[Interruption]

[Laughter]

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Frankline Makanga, I think you have to withdraw that.

Hon. Makanga: Mheshimiwa Spika itakua ni makosa kama nitakubaliana na yale wanasema kwamba ni *withdraw*. Mheshimiwa Spika, labda nieleze kwamba wasiozungumza inaweza pia kuwa wale wana uwezo wa kuzungumza lakini kwa muda mwingi tumekuzoea huzungumzi...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Mheshimiwa Frankline Makanga, hayo si majukumu yako wewe kama Mheshimiwa ukiwa umekaa hapo kuja kutuambia ni nani anazungumza na ni nani hazungumzi. Kwa hivyo ningeomba ufuatilie mbali usemi wako uendele.

Hon. Makanga: Ahsante kwa muongozo wako Mheshimiwa na kwa ajili ya kuwalinda wenzetu ambao kwa mara nyingi hawataki kuchangia wacha niombe msamaha. Nafuatilia mbali usemi wangu.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you. you can continue.

Hon. Makanga: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa hivyo...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): So, you have withdrawn and you have given apology?

Hon. Makanga: Kabisa nishafanya hivyo Mheshimiwa...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Ahsante.

Hon. Makanga: Ahsante. Mheshimiwa Spika ndio mimi ilikua najaribu kujenga hoja yangu na labda nikimalizia ni kwamba, mimi ningeomba jambo hili la utenda kazi wa hospitali zetu na taasisi zote za kiserikali tusizifanyie siasa, in English let us not use our institutions for public relations. Mombasa residents elected us to offer leadership and offer solutions where there are problems. It is high time that we as a government, both the Assembly and the Executive we come out of comfort zone and offer leadership and solutions to the challenges affecting our people and it stands now Honourable Speaker it is my humble request that every leader in Mombasa desist from politicizing this issue and be ready to offer solutions, guidance and leadership so that our people would be able to get the best of services; as a Member of Health Committee Honourable Speaker, I want to give my highest assurance that we shall go to the bottom of this matter and of course we shall be messy with casualties. Thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Frankline Makanga. Yes, Honourable Juma Manuari from Bofu Ward please make your contributions.

Hon. Juma Manuari: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo. Pili, nirudishe shukrani kwa viongozi walioko ndani ya Jumba hili, kukaa chini na...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Khatri): Order! Order Honourable Members please!

Hon. Juma Manuari: Kukaa chini na kuchachua hoja hii ambayo imeletwa na ndugu yetu Mheshimiwa Allen, kuhusiana na mtendaji mkuu wa hospitali yetu kuu ya Pwani. Mheshimiwa Spika hivi sasa tunajua tuna miamko mingi sana, lakini kaka yangu, ndugu yangu Mheshimiwa Allen ameleta mapendekezo ambayo ni muhimu kufuatiliwa na sisi kama viongozi ndani ya Jumba hili, tusiwe wa kwanza kusimama na kurusha dongo ama kulaumu mtu, wakati mwelekeo kwa sharia na kikatiba ya nchi upo. Ikiwa ndugu yetu ameleta mapendekezo akasema majopo yaundwe, Kamati ziundwe, mwelekeo uundwe, uchunguzi na kuangalia jinsi gani mtendaji mkuu ndugu yetu Iqbal yale matatizo yalitokea juzi ni ya kweli ama ni ya uongo. Ni yake ama si yake? Tukijua fika kuwa uhai ni wa Mwenyezi Mungu, kuishi ni Mwenyezi Mungu. Huenda ukawa hii ni sababu tu ya kuwa pengine alipiga simu kiongozi yule na simu yake

haikusikizwa, hio wakapata sababu ya kumsukumia Iqbal maneno na si yeye kuwa atakuwa ni mhudumu yuko ndani, na si yeye kuwa atadunga mtu sindano ama atafanya nini. Yeye ana majukumu yake binafsi. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika kabla hatuja muamulia mtu na tukasema ni mbaya ana rangi ya chui ama rangi ya nini ama yale yote yanayozungumzwa, mimi napendekeza hata mimi hoja zilizotolewa na ndugu yangu, watu wakae chini, jopo lifanye kazi yake, uamuzi uletwe ndani ya Bunge hili, sasa yale mapendekezo tutayatoa baada ya matokeo ndio tutakaa na Gavana, na yule mhusika yeyote tufanye maamuzi yao. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika yangu ni hayo kwa sasa ahsante sana.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Athman Mwamwiri? Please make your contribution.

The Leader of Majority Party (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika, nimesimama kuunga mkono hoja hii ya kwamba Kamati ya maswala ya Afya na Matibabu waweze kuvalia njuga swala hili na kuleta ripoti katika Bunge hili, kutokana na yale yanayoendelea katika hospitali yetu almaarufu, Hospitali ya Makadara. Lakini yale aliyoleta Mheshimiwa Spika kuna Waheshimiwa katika kuchangia kwao wamehoji swala la mamlaka ya kupeana ridhaa ya kufutwa kuabili katika hospitali ile na kwamba jukumu hili ni la nani. Kwa mujibu wa sheria Mheshimiwa Spika, sheria ya maswala ya fedha ama PFM Act, sehemu ya (159) mamlaka ya *waiver* yako chini ya waziri wa fedha. Mheshimiwa Spika vile vile Makadara ama Hospitali yetu Kuu ya Mkoa wa Pwani ya maswala ya mafunzo, inasimamiwa na halmashauri ama *'Board'* ambayo halmashauri hii iliundwa kwa mujibu wa sheria ya Bunge hili ambayo msimamizi mkuu ama ofisa mkuu, ana wajibu wa kujibu moja kwa moja kwa bodi ile ama almashauri ile. Mheshimiwa Spika kwa mamlaka ya Bodi hii kama ilivyo Bodi zingine zozote na hata ukisoma *County Government Act* sehemu ya (62) inapeana mwongozo wa mamlaka inapokuja swala la wafanyikazi na adhabu kwa mfanyikazi. Mheshimiwa Spika, kwa hivyo Bodi katika kutoa ilani ya kumsimamisha kwa ajili ya uchunguzi mfanyikazi yule ambaye ana jibu kwao, walikuwa sahihi lakini vile vile kwa aliyesimamishwa sheria imemlinda ya kwamba ana haki ya kupewa fursa ya kujieleza, fursa ya kujitetea na kama haki hii haitatekelezwa basi ana haki vile vile ya ku *appeal* kwa tume ama kwa *Public Service Commission* ya kitaifa iwapo sheria haijafuatwa.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika sisi jukumu letu kama Bunge, na swala la nidhamu kwa wafanyikazi vile vile pia, limeangaziwa katika *PFM Act* sehemu ya (74) ya kwamba kila mfanyikazi ana wajibu wa kubeba msalaba wake binafsi, kwa matendo yake binafsi lakini haya yanapo tekelezwa tunakuja tu katika lile swala wataalam wanaita, *"Principals of Natural Justice"* kwa kina Mheshimiwa Hossana ambaye amesoma sheria, wanalifahamu zaidi hili kutuliko sisi ambao tumesoma tumewekeza zaidi katika sayansi ya siasa. Mheshimiwa Spika na hii inapeana ya kwamba ndugu yetu CEO Khandwalla bado ana haki zake za kimsingi kwa majukumu aliyokuwa akitekeleza na Kamati hii tunapo ipa mamlaka na fursa ya kutekeleza haya kufuatilia, vile vile tunawasihi ya kwamba wazingatie sheria kwa sababu, imedhihiri katika Bunge hili miongoni mwetu na tunalijadili swala hili kwa jazba wakati ukweli wa jambo lenyewe haijasimama wala kuyakinika kwa hivyo pia Waheshimiwa niwaombe hususan Kamati katika utekelezaji wa jukumu hili tutekeleze kwa misingi ya kisheria.

Kwa sababu sisi ndisi watunzi wa sheria Mheshimiwa Spika na tuhakikishe ya kwamba ripoti yetu imeangazia matakwa ama mapendekezo ambayo ndugu yetu aliyeleta hoja hii, ametaka ili kupatikane usawa lakini vile vile iweze kulindwa haki ya kimsingi ya wananchi kwa sababu hii inatupatia mamlaka ama inapeana nguvu swala lolote ambalo lina mapenzi ama *interest* ya wananchi Mheshimiwa Spika, wakati mwengine pelekea maamuzi magumu

kuchukulika kwa haraka na sheria kufuatwa baadae. Kwa hivyo hayo yote Mheshimiwa Spika yaweze kuwekwa katika mizani ili isiwe tu ni kisingizio cha kuepuka malawama mengine, lakini iwe ni sababu ya kuweka sawa taasisi zetu zote za serikali ya Mombasa, si tu za afya lakini mpaka zile za elimu, za maswala ya biashara ya kwamba sheria inafuatwa, huduma kwa wananchi wa Mombasa inapatikana inavyostahiki na yeyote atakae patikana amezembea basi sheria ifuate mkono wake. Kwa hayo Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja hii ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Athman Mwamwiri. Yes, Honourable Maryam Baimu? Please make your contribution.

Hon. Baimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuweza kunipatia nafasi hii. Mimi nimesimama kuunga mkono hoja hii na kusema ile ukweli japo kuwa tumepewa ama ile Kamati ya afya imepewa majukumu ya kuweza kufuatilia jambo hili, lakini pia ni muhimu sisi kama viongozi hapa ndani tuweze kupeana hoja moja ama mbili ambazo ule ukweli hali vile ziko pale hospitali ili waweze kuchukua na wao katika hizo *findings* zao waweze pia kuongeza ili yale watakao pata kule nje na yale yatakayo kuwa tumepewa sisi, ndio hapo watakapo tuletea ripoti yetu iwe ni ripoti ya kueleweza. Mengi yameongelewa lakini kwa uchache sana mimi kusema ule ukweli shida kuu ambayo mwatafikana muangalie Kamati ni ule upande wa SHA, kama vile ilivyoongelewa ni donda sugu. Pale, mgonjwa huwa haambiwi kuhusu SHA wakati anapoingia anaelezwa wakati anatoka na wakati huo itakuweco *bill* iko juu ya kwamba yule mgonjwa sasa anatukimbilia sisi Waheshimiwa ama mimi Mheshimiwa upande wangu Frere Town ili wakiomba usaidizi. Kusema ule ukweli Mheshimiwa Spika hii shida ya *bill* kubwa pale Coast General imekuwa donda sugu na kusema ule ukweli kama ile *waiver* ya miaka mitano kwenda chini ile haiko kabisa. Nafikiria Mheshimiwa Spika ili jambo likisha tatuliwa vizuri mambo yarudi vizuri pale upande wa ma *bills* nafikiri hata wewe Mheshimiwa Spika utapumzika manake sisi sote hapa tukija kufuatwa manyumbani na ofisini kuhusu *bills* watu wamekwama si za hospitali wala za *mortuary*. Mnyonge wetu wa kukimbilia ni wewe Mheshimiwa Spika.

Kwa hivyo imani yangu hapa ikiwa itatatulika ili ipatikane njia mwafaka kuhusu hizi *bills* zirudishwe chini, kuhusu hizi *waiver* ziweze kutekelezwa kama kawaida ni *bill* iko kubwa hiyo *Waiver Committee of Coast General* iweze kuangalia vizuri manake tunaamini mtu mwenye pesa zake hawezi kwenda Coast General kutibiwa atakwenda Aga Khan, Mombasa Hospital, Pandya lakini si Coast General. Kwa hivyo mimi imani yangu wanaokwenda pale ni watu ambao ni wanyonge na wanahitaji matibabu, waki *expect by the time* wanatoka *bills* zitakuwa ndogo waweze kulipa. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika kusema ukweli kando na mambo ya SHA waangalie hawa wanaokwenda kutafuta utafiti, kando ya hizo mambo ya *waiver* pia wale wafanyikazi wengine kando ya Khandwalla, kwa sababu Khandwalla yeye ni mkubwa pale na hawezi jua pengine wafanyikazi wake wanafanya mambo gani, lakini pale kusema ukweli service huku chini ni mbaya sana. Nikizungumzia tu kwa uchache mfano kama *maternity* leo naongelea kuna mgonjwa wangu wa Frere Town, ameachiwa saa hii inaenda wiki pale *maternity* na amefanyiwa *caesarean* na bwanake ako na SHA na hakupeleka mapema pale, sasa yule amelazwa mtoto mpaka anageuka macho *yellow* ananililia mimi nimsaidie. Mheshimiwa Spika, nimemsumbua sana na *bills* mpaka sasa hivi naona aibu kukufuata na mambo ya *bills*, inabidi sasa nifuate yule Waziri Swabaha. Nikimfuata Waziri Swabaha naye jibu lake analo nijibu yeye kama ni Coast General niweze kupiga mwenyewe simu kwa *Director* manake yeye ameshindwa na uongozi wa pale Coast General. Sasa Mheshimiwa Spika ikiwa Waziri wa Afya anashindwa kutusaidia sisi ili wananchi wetu waweze kupata huduma kusaidika, wakati wanatoka hospitali waziri anasema hawezi ameshindwa, je Mombasa tunaeeleka wapi? Kwa hivyo kimimi naomba hii Kamati ya Afya muweze kuchunguza vizuri, mupate jibu za kueleweka

mtulete hapa, tuchambue ndio tujue kama kweli Khandwalla anapaswa kwenda nyumbani, ama Khandwalla aweze kuregeshwa kazini, ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Salim Mbaya?

Hon. Salim Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa nami niweze kuchangia hoja hii ambayo ni muhimu. Mheshimiwa Spika kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu na pili nimesimama kuunga mkono hoja hii ya kwamba, Kamati ya maswala ya matibabu ama maswala ya afya, iweze kufanya uchunguzi kwa sababu siku zote hukumu ambayo itatolewa kabla ya kupeanwa ushahidi, Mheshimiwa Spika itakuwa ni dhuluma. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika mimi naona cha msingi zaidi kutokana na hoja hii ambayo imeletwa na ndugu yangu Mheshimiwa Allen Katana, itakuwa bora Kamati ya Afya iwe itaingia kwa kina kufanya uchunguzi kuona ya kwamba hizi hali ambazo zimeweza kutokea Coast General matatizo haswa yanatoka wapi na wawe na ushahidi ili kama ni hukumu kutolewa, iwe ataadhibiwa yule ambaye anastahili. Mheshimiwa Spika, ndio Iqbal Khandwalla ndiye ambaye ni msimamizi wa hospitali, lakini uchunguzi inawezekana labda pengine labda kuna amri ametoa na haikutimizwa na hukumu ikatoka kwake lakini ikiwa kutakuwa na uchunguzi ama upelelezi wa hali ya juu, ule ukweli utakao patikana ndio ambao utaweza kuchukuliwa hatua. Mheshimiwa Spika, nimesimama kuunga mkono kwa asilimia 99 kuona Kamati ya Afya imeweza kufanya uchunguzi wa kina. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Mwaura? Please make your contribution from Kongowea Ward.

Hon. Mwaura: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuniona na kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu ambayo iko mbele zetu. Mheshimiwa Spika kilio cha watu wa Mombasa kwa hakika kimezidi, na ndio sababu kila asimamae anaunga hoja hii mkono, na mimi sina budi ninaunga mkono kwa sababu Kongowea imo ndani ya Mombasa na Mombasa inaumia kwa sababu ya swala hili. Mheshimiwa Spika cha kuongezea katika haya maombi ambayo yameombwa nataka kupendekeza ni muhimu sana madai ambayo yamekuja, kuna madai ambayo tumeyasikia sana na labda sijaangalia vizuri lakini madai yanayo husiana na magonjwa maalum na madaktari kuuliza wagonjwa ya kwamba magonjwa maalum wayapeleke kwa kliniki zao ili na ni magonjwa kama upasuaji na magonjwa mengini, ili waende kwa kliniki zao na kutengeneza fedha uko na ninashangaa, kliniki hizi ndogo zitawezaje kuwa na vifaa vizuri zaidi kuliko hospitali yetu ya Makadara. Kwa hivyo mimi naunga hoja hii mkono na ninasema pia waangalie ile tunaita ya nurse to patient ratio iko namna gani? Na kama wengi hawaendi kazi wamezembea ili kazi iendeleo kulala na naunga mkono hoja hii Mheshimiwa Spika, ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Mwaura. Yes, Honourable Morgan Matsaki?

The Leader of Minority Party (Hon. Matsaki): Nashukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii; pili, nimesimama kuunga mkono hoja hii na tatu pia Mheshimiwa Spika namshukuru Mheshimiwa mwenza Mheshimiwa Allen Katana kwa kuleta hoja hii na mapendekezo ambayo amepeana kwa hii Kamati yako wazi, ambayo mapendekezo matano sitayaregelea kusoma kwa sababu tayari yashagusiwa na langu la muhimu hasa kwanza. Mimi huwa nasema kwamba Kamati imepewa tu siku saba kulingana na mapendekezo ya Mheshimiwa aliyeleta hoja hii; siku saba hizi Jumba hili tuko tayari kusikiza hoja ambazo zitakazoletwa na

Kamati na tuone kweli ule uzembe unaozembewa pale kwa ile hospitali, tuweze kuchukua hatua mwafaka tuweze kutatua jambo hili. Mheshimiwa Spika, nimesimama kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Ojala Pamela?

Hon. Ojala: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity also to give my contribution. Mr. Speaker, I stand to support the Motion; *Investigation into the Management and operation of Coast General Teaching and Referral Hospital*. I want to thank the mover of Motion for bringing this important Motion to this Honourable House. It is well stated in Article 41(1) of the Constitution of Kenya Mr. Speaker, that every person has the right to have a better health and if you look at the five prayers that the mover of Motion suggested, when you check at number five, our hands are tied to debate this Motion today, until the Committee comes up with a comprehensive report. Mr. Speaker *Waswahili wanasema, "Mgala muue haki yake mpe"*! Most of us do not have a story with the Coast General if not Mr. Khandwalla the Coast General would have not been the Coast General of today. Mr. Speaker, I stand to support the Motion. Thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you. Yes, Honourable Mose Joshua? Please make your contribution.

Hon. Ong'au: Thank you Mr. Speaker for also giving me an opportunity to support this Motion, the pleas of the mover of the Motion are very clear and lastly Honourable Speaker, I am requesting that you take some of our Members for induction so that we can debate positively, we know what are the pleas of the Motion, what is required of us to debate, by talking too much we add zero. Thank you.

[Applause]

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Joshua Mose. Yes, Honourable Patrick Mbelle?

Hon. Mbelle: Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mwenza kutoka Shanzu shemegi yangu kwa kuleta hoja hii na Mheshimiwa Spika niombe kwamba tunapofikiria hoja hii naomba kidogo, tukue kwa kizungu wanasema "*selfish*" tukue wachoyo kidogo na tukumbuke kwamba sisi leo hii ni Waheshimiwa lakini itafika wakati ambapo tutaacha viti hivi na tutakuwa wananchi wa kawaida, labda kwa kupenda sisi wenyewe ama kwa wananchi kuamua kwamba hatutakuwa Waheshimiwa katika Bunge hili. Wakati huo utakapofika Mheshimiwa Spika, hatutakuwa na uwezo wa kuwa na zile bima ambazo tuko nazo leo, zinaturuhusu kwenda Aga Khan. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika tunapopea Kamati ya Afya nguvu na nafasi ya kuweza kufanya uchunguzi kuhusiana na Coast General, tukumbuke ya kwamba siku moja pia sisi tutakuwa wagonjwa ambao tungeweza kuitaji kutumia hospitali ile na hatungetaka kutumia hospitali ile, ikiwa katika hali ambayo haitoi huduma nzuri si kwa mwananchi kwa sasa bali mwananchi wakati wa kesho.

Mheshimiwa hoja hii inanikumbusha katika vitabu vya historia wakati wa utawala wa Hitler kule ujerumani kuna mfungwa mmoja alipotoka akasema mara ya kwanza walikujia wasosholisti na sikusema kwa sababu sikuwa msosholisti, wakakujia wanaharakati na sikusema kwa sababu sikuwa mwanaharakati, tena wakakujia wa yahudi na sikusema sababu sikuwa

Myahudi, lakini ikafika mahali walipo nikujia mimi nikatafuta wa kunisemea lakini hakuna wa kunisemea aliyekuwa kwa sababu wote walikuwa wamefungwa. Mheshimiwa Spika wakati huu tuko na nafasi ya kuweza kuleta mageuzi katika hospitali ya Coast General. Wakati huu Mheshimiwa Spika tuko na nafasi ya kuweza kuangalia huduma ya Coast General inaweza kuwa bora kuliko vile ilivyo sasa ningeomba kwa tafadhali Kamati ya Afya ingawaje inaonekana kana kwamba tumechelewa katika kuleta hoja hii, lakini kuna umuhimu mkubwa kuhakikisha ya kwamba, Hospitali ya Referral ya Coast General inaweza kutoa huduma bora na sio huduma tu kwa sababu inafaa itoe huduma.

Vile vile Mheshimiwa Spika ningeomba tuweze kufikiria kitu kimoja, kweli ninachoongea saa hizi inaweza kuwa nje ya mada, lakini kuna wakati ambapo hospitali kama hii ya Coast General ile ya Kisumu, nafikiri inaitwa Jaramogi Oginga Odinga Teaching and Referral Hospital Mheshimiwa Gavana wa Kaunti ya Kisumu Professor Anyang Nyongó aliamua ya kwamba hospitali ile aipeleke kwa Serikali Kuu ili iweze kuwa *managed* na Serikali Kuu, Mheshimiwa Spika Hospital ya Coast General leo hii inabeba wagonjwa kutoka Tana River, Kilifi, Kwale, inachukua wagonjwa kutoka sehemu zote za Kenya. Mheshimiwa Spika bajeti ama mgao wa Serikali ya Kaunti ya Mombasa, haitoshelezi huduma na matakwa ya hospitali ya Coast General ni wakati ambapo mnapoenda kufanya uchunguzi na kuleta *findings* katika Bunge hili, ningeomba endeni mukafikirie ni vipi hospitali hii tunaweza kuipeleka kwa Serikali Kuu ili Serikali Kuu iweze kuhuduma hospitali ile na itoe huduma kwa watu wetu wa Mombasa. Mheshimiwa Spika tuweni wa kweli katika nyoyo zetu, Hospitali ya Coast General ki ukweli Kaunti ya Mombasa peke yake, haiwezi kuithibiti na kuimiliki na kuweza kuhudumia wananchi ambayo wanakuja katika Hospitali ile. Kwa hivyo tunaweza kuwashtumu, tukawalaumu, tukakashifu tukafanya mengi lakini Mheshimiwa Spika, leo ndio nafasi ya sisi kuongea na isifike wakati katakuwa na mtu wa kutuongelea, wacha leo tuweze kuongea na tuongee ukweli na tuhakikishe ya kwamba watu wetu wanapata huduma ambayo inafaa. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Kharti): Thank you very much. Honourable Patrick Mbelle from Bamburi Ward. Honourable Samir Bhalo from Tudor Ward please make your contribution.

Hon. Bhalo: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Ni jambo la kusikitisha sana, hatuzungumzi mambo ya jana wala juzi, ni mambo ya leo asubuhi tulipokuwa hospitali ya Coast General tukimtoa mwanamume mmoja ambaye alikuwa pale kuanzia mwaka uliopitana alikuwa amemaliza matibabu. Ni jambo la huzuni sana huyo mzee ana miaka 90 alikuwa hana uwezo wa kutoka leo asubuhi nikajaaliwa tulim *release*. Mheshimiwa Spika, Coast General kule kwetu tunaita kichinjio utaingia na miguu yako na utatoka kwenye sanduku ama sanda. Sio jambo la kuambiwa wala sio stori Mheshimiwa Spika mwaka jana tarehe saba mwezi wa saba, mtu wangu wa karibu sana alikuwa Coast General, Mheshimiwa Spika kwenye ile Wadi kulikuwa na watoto wawili ambao waliungua na maji ya moto kuingia kama saa sita wale watoto walikuwa wanalia na njaa nikauliza wana shida gani, yule mama mmoja wao akaniambia kuwa chakula hakijaletwa mpaka sasa. Mimi nikaondoka pale nikaenda kwa wadi ya yule mtu wangu wa karibu wa palepale, kuanzia saa kumi na mbili asubuhi wale watoto walipewa mayai mawili na slesi mbili za mkate nikakaa pale hadi saa nne usiku Mheshimiwa Spika wale watoto ama nusu ya hospitali hawakuletewa chakula. Nikafuatilia mimi binafsi kuja kuambiwa kuwa gesi ya hospitali imeisha. Hiyo ni tarehe saba mwezi wa saba mwaka 2025 siwezi kusahau ile siku, yule mama alitaka kuleta chakula ndani alikataliwa, Mheshimiwa Spika leo tukiangalia ukienda coast general mtu wa kawaida hukuibaliwie kwenda na simu wala kupiga picha pale maana kuna uchafu mwingi pale hawataki watu wa nje waone, Mheshimiwa Spika leo nimesimama kuungana mkono na

ndugu yangu Katana kuwa huduma ya matibabu ya Coast General lazima yarekebishwe maana pale lile jina la kichinjio limeitwa na ni kweli. Ahsante sana.

The Speaker (Hon. Kharti): Thank you very much. Honourable Samir Bhaloo. Yes, Honourable Samir Bhaloo.

[Interruption]

Yes, Honourable Leila Nyache from Kipevu Ward, please make your contributions.

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi kuweza kuniona. Nimesimama kuunga mkono hoja hii iliyoletwa na Mheshimiwa mwenza Allen Katana, kwa kweli kila mtu ametoa hisia zake hapa, hisia zote zimetolewa zote tunajua ni za kweli, mimi ni mmoja wapo pia ambao pia nilikuwa na mgonjwa pale Makadara na nilikaa karibu wiki tatu, wiki tatu hizo ile *bill* ilikuja kubwa sana hata nilishangaa kuna rafiki yangu mmoja, alikuwa amekuja kumuangalia mgonjwa wangu alikuwa mkaza mwana, akaniambia hii *bill* ilikuja elfu mia moja na sabini imetoshana na ile mwanangu alikaa pale Mombasa Hospital kwa wiki nne na nikatoa elfu mia moja nane karibu zitoshane. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika upande wa *bill* tuangalie sana kwa sababu wanyonge ndio wanaenda kwa ile hospitali, wajaribu upande wa *bill* washukishe ambapo itaweza kusaaidia watu na mimi pia nashukuru Mheshimiwa Spika yule mgonjwa wangu uliweza kumsaidia akatoka, hilo pia nakushukuru sana. Kitu nitasema hoja imekuja leo ni tuunge mkono Kamati husika ambao ni wa Afya waweze kuiangalia hivi vigezo, kuna vigezo vitano vimewekwa hapa. Waweze kufuatilia na waweze kuja na ripoti nzuri ambapo tutaweza tupate suluhisho kamili kuhusiana na mambo yaliotokea Coast General. Tusinyooshe kidole kwa upande mmoja peke yake, tunaangalie upande huu na ule ambapo tunaweza tunakuja na suluhisho, ndugu yetu labda Khandwalla yeye labda ni siku hiyo ambapo amekataa kushika simu ama labda imetokea na mtu siku yake imefika, inaweza kumuangukia kibao kikawa yeye ndio mkosa mkubwa ama yule ndugu yetu aliosema hakushikiwa simu, hatujui ni yupi ni yupi, yatakikana tuangalie huku na huku hayo makosa yaweze kurekebishwa. Lakini kwa upande wa *bill* naomba Coast general waweze kushukisha *bill* kwa sababu hospitali ile wanyonge ndio wanaoenda waweze kuweza kulipa ile bill na kutibiwa. Ahsante Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono.

The Speaker (Hon. Kharti): Thank you very much Honourable Leila Nyache. Yes, Honourable Maimuna Salim. Please make your contributions.

Hon. Maimuna Salim: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono hoja hii iliyoletwa na Mheshimiwa mwenza; yangu ni masikitiko kwa sababu tumelia mda mrefu sana lakini sikitiko langu ni kwamba sisi kama Wabunge wa Kaunti tumekuwa kama *simba sarakasi*. Kwa sababu ya kusema hivo ni kwamba, sisi ndio tulikuwa tulie na tuhakikishe ya kwamba Kamati ambayo ni ya afya Mheshimiwa Spika langu ni masikitiko kwa sababu mimi mwenyewe kibinafsi nishawafuata nikiwaelezea kuna matatizo kama Mheshimiwa mwenza kama mwezi wao lakini niliona kwamba kuna vile ambavyo kazi zinafanywa. Kwa hivyo sisi Kamati tulikuwa tunaamini na mpaka sasa sio eti hatuiamini lakini tunaomba washirikiane na sisi Waheshimiwa wenza kuhakikisha kwamba wamefanya kazi yao kama Kamati hakuna cha kuficha wala cha kukunja kwa sababu sisi tuko hapa kuwakilisha wananchi wa Mombasa na eneo la pwani kwa ujumla kwa sababu Makadara...

[Interruption]

The Speaker (Hon. Kharti): Honourable Salim Mbaya.

Hon. Salim Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kunipatia fursa hii. Mheshimiwa Spika nimesimama kumtaka Mheshimiwa mwenza atufafanulie katika Nyumba hii Mheshimiwa ambae ni *simba sarakasi* ni nani, kwa sababu vile nafahamu wale ambao wako kwa Nyumba hii wale ambao ni wa kuchaguliwa na chama walitambulika walifanya kubwa kazi sana ndio chama kikawatambua na wale ambao walichaguliwa na wananchi kulikuwa na wengi ambao wamesimama lakini wakatambua hawa ambao tunachagua ni watu ambao wako imara wako thabiti tunawaamini Leo hii Mheshimiwa anasema Nyumba hii kuna Waheshimiwa mbao ni *simba sarakasi* naomba afafanue hilo Mheshimiwa Spika.

Hon. Maimuna Salim: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nimesema hivyo manake tuko hapa tuna mambo mengi ambayo tunajadili katika Bunge hili, na hakuna yani utekelezaji kwa upande wa *executive* na sisi tumenyamaza na nimesema hivo ndio maana nimesema hivo nimesema kwa uchungu kwa sababu ni mambo mengi na kusema kweli kwa upande wa *executive* hakuna kitu chochote ambacho chafanyika ndio maana nimesema hivyo. Mheshimiwa Spika mimi nimesimama kuzungumza ya kwamba kamati husika iweze kuhakikisha ya kwamba itakuwa ni kazi iweze kufanya na ilete majibu kamili kwa manufaa ya watu wa Mombasa na wa pwani kwa sababu watu wengi Mheshimiwa Spika, tunalia na tunakuja kwako unatusaidia ushatutolea miili *mortuary*, ushatusaidia na bili ambayo tumeshindwa kwa hivyo ni lazima kuwe kunao ufuatiliaji, alafu jambo lengine ambalo pia nitaomba kamati ikikaa isisitize kuna watu pale hawawezi hata kuinua mkono, lakini ukizungumza kwamba alale na mtu madaktari hawataki na nurse kwa sababu kuna vitu wanaficha wao ikifika usiku wanalala, wanafanya shughuli zao, wagonjwa kule wanataataa wakiwa pekee yao kwa hivyo hilo pia liangaliwe. Mimi langu kubwa ni kuomba Kamati husika iweze kufanya uchunguzi na ituletee ripoti ambazo ziko za kikamilifu, Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono hoja hii na nakushukuru sana kwa msaada wako mkubwa maana wewe ndio umekuwa baba yetu na imekuwa kila kitu tunalia kwako, kwa hivyo tunaomba Kamati husika iweze kuchukua nafasi kufuatilia na hata sisi wengine tutakuwa *watchdog* wa kufuatiliza huko nje. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Kharti): Thank you very much Honourable Maimuna. Yes, Honourable Florence Kachumbo.

Hon. Kachumbo: Thank you Mr. Speaker for this opportunity. I would like to congratulate Honourable Katana for this audacious thing that he has done, I have been in a certain forum where one of the doctors was complaining about being underpaid so it is good that the Committee does a thorough investigation because it's not just the condition but also some workers are really underpaid and they cannot be productive, so i would ask the Committee to do a thorough investigation and come up with solutions for the people of Mombasa because it's such a sad situation. Thank you.

The Speaker (Hon. Kharti): Yes, Honourable Hamida Noor please make your contributions.

Hon. Noor: Thank you, Mr. Speaker, for giving me the opportunity. I stand to support the Motion but Mr. Speaker I have some few remarks on my own; sometime last month we had a

patient there who really had a rough time when we took him there, but the services that we incurred there were not really to our standard because when we brought in the patient, the patient had a heart problem and then in there he developed a kidney failure, but the doctors did not come and see him in time, Mr. Speaker and unfortunately after two days he passed on Mr. Speaker, for me to stand up here and narrate these stories, it is very hurting because I'm the one who is giving the legislation here, I'm the one who is standing in this County Assembly and giving out the legislation and the services that we are getting is not to our standard. Mr. Speaker, what we really need is to pick up the services with our patients in there because the way you have heard is that most of the Members here are complaining mostly about the services that are being given at the hospital. With those few remarks, Mr. Speaker, I do stand to support the Motion. Thank you.

The Speaker (Hon. Kharti): Thank you very much, Honourable Hamida Noor. Yes, Honourable Bernard Ogutu from Changamwe Ward and the Chair of Health Committee.

Hon. Ogutu: Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker, as I stated in the morning, we had scheduled a meeting as a Committee guided by Article 195 of the Constitution and the schedule is as follows; tomorrow at 11:00a.m. We will be meeting the victims, on Friday at 10 a.m. we'll be meeting Coast General Teaching and Referral Board and the Department of Health, on Friday at 2:00p.m. we will be meeting the suspended CEO and the doctors who were involved in this matter at hand. Mr. Speaker, as the Chair of Health, I want to remain objective and I will not make any political declaration here as the Article is very clear, the sitting of a County Assembly Committee is equated to a sitting of High Court so, there are some things that is expected of us that as a Committee we cannot say here. We will go deep down the matter and bring a conclusive report over this issue. Number two, Mr. Speaker, seven days may not be sufficient but we will try to work within the seven days. If need be, we'll request for additional time. Thank you.

The Speaker (Hon. Kharti): Thank you, Honourable Ogutu. So that was an invitation for the Members or did you invite the other Members as well?

Hon. Ogutu: Mr. Speaker, I want to take this opportunity to invite all Members to attend. Thank you.

The Speaker (Hon. Kharti): Thank you very much, Honourable Bernard Ogutu, Chairman for Health Committee. Yes, Honourable Allen Katana, please reply to the Motion.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika nichukue nafasi hii tena kwa mara ya mwisho hii leo kushukuru Waheshimiwa kama walivyotoa hekima yao kwa ajili ya swala hili; katika maombi haya Matano kama Waheshimiwa wote walivyo yapitia ni kama Waheshimiwa, Mheshimiwa nataka niwaeleze Waheshimiwa wengine ambao wanajisikia wamekwazwa, katika changizo za Waheshimiwa ni kwa sababu hawako hapa kwa sababu za kisiasa wako hapa kufanya moja wa majukumu yao ya *oversight*, ikiwa unahisi watu wako wanadhulumika ni haki yako kusema, ikiwa kusema kwako inaonekana ni siasa wacha siasa iendele maana hata siasa ndio imetuleta hapa. Mheshimiwa Spika na baadhi ya sababu zilizo nifanya zilizo nifanya kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu 2027 huenda hamtakuwa na mimi ni kwa sababu kuna sheria zengine nataka na mimi kwenda kuziweka katika Jumba la kitaifa ya kwamba hawa Waheshimiwa ambao wanaogopa kutetea watu wao nataka kwenda kuwawekea sheria *cover* zao ziwe ni za hospitali za serikali kama Makadara, Kenyatta Hospital na sio zengine, ili kile wananchi wetu wanapitia sisi Waheshimiwa vilevile tupitie, ndio maana hatutaita mambo ya kutetea watu wetu kuwa siasa.

Mheshimiwa Spika kitu chengine ni kwamba nikimaliza inanistajabisha Mheshimiwa Rais anapokuja Mombasa sisi akija huku ni *two term* akienda kule bara wenzetu wanaomba vitu na wanafanyiwa, sisi huku ni *two term* na ilhali ripoti zinasema Makadara SHA inadai over 700 million. Sasa wewe unaimba *two term* na ilhali kuna pesa, mwambie Mheshimiwa Rais kwamba tetesi zinasema SHA haijalipwa Makadara pesa kadhaa. Sisi tutaendelea kusimama na mwananchi iwe ni daktari Khandwalla ana makosa, iwe hana makosa sisi kama Jumba tutasimama na pale haki iko ili mwisho wa kwisha watu wetu wakaweze kupata matibabu.

Mheshimiwa Spika hili lilinihuzunisha sana, mimi kwa wanao nijua Mheshimiwa Spika ni Mgiriama *pure high breed* hii kukonda ni kwa sababu ya asthma Mheshimiwa Spika, lakini Mgiriama mimi nimeoa kule Asembo mke wangu ni Mjalu Mheshimiwa Spika, kilicho nihuzunisha ni kauli za kiongozi akisema muhindi, hata vitabu vya dini vinasema kama wewe ni mzinifu sema mimi ni mzinifu Allah nisamehe utasamehewa. Tusilete maswala ya ukabila ndani ya mtu unayemkisia kwamba amefanya ikiwa dhambi imefanywa na daktari Khandwalla sema Khandwalla lakini maswala ya uhindi na kuweka mambo ya kikabila Mombasa yetu ni *cosmopolitan region* na mambo ya vita ya kikabila tumeviona vimetuchosha. Mheshimiwa Spika la mwisho kuna Mheshimiwa hapa ambae hua anajisifu sana na mambo ya kutufunza sisi Kiswahili lakini leo amesema akasema interest ni mapenzi nataka kumfundisha Mheshimiwa Mwamwiri *interest* ni maslahi na kama huamini rudi shule usome sio Mapenzi...

[Laughter]

Waheshimiwa ni washukuru sana kwa kuunga mkono swala hili katika vikao nilivyokaa Jumba hili. Mheshimiwa Spika kama kuna kitu tumekizungumzia na kiko ndani ya moyo wangu ni maswala ya matibabu ya watu wetu. Mheshimiwa Spika yuko Mheshimiwa ameongea na jambo likamgusa moyo wake mpaka kidogo kukaingia maneno makali kusema Makadara ni kichinjio. Hivi sasa kuna wagonjwa wako pale Makadara tukisema pale ni kichinjio na kuna matumaini ya kwamba watapona kuna wengine tumewaua, Mheshimiwa Spika nataka kusema kwa kuwa huyu Mheshimiwa ni msilaumu na anatarajia kutakuja sikukuu ya kuchinja alikuwa ameashiria hiyo siku ya kuchinja na sio eti Makadara ni kichinjio. Kwa hayo mengi Mheshimiwa Spika niwashukuru na muwe na Ramadhan Kareem. Ahsante.

[Applause]

The Speaker (Hon. Kharti): Thank you very much Honourable Katana *IGB* and the Honourable Members of the County Assembly for your contributions. It is now time for me to put the question that the Motion by Honourable Allan Katana be approved by this Honourable House in the same terms as moved or as debated?

[Question put and agreed to]

The Motion by Honourable Allan Katana is adopted by this Honourable House.

ADJOURNMENT

Honourable Members, this House stands adjourned until Wednesday, 25th of February, 2026 at 10:00a.m.

The House rose at 4:29p.m.